

TOLEO LA. 07

Jarida la *Ni Magufuli Tena*

2020 - 2025

ALIAHIDI | AMETEKELEZA | APEWE TENA 5 | 6 SEPTEMBER, 2020



KARIBU MWANZA DKT. JOHN POMBE MAGUFULI



Limeandaliwa na **TEAM MAGUFULI TENA**



MAGUFULI: TUMETEKELEZA AHADI KIKAMILIFU WILAYA YA MAGU

Na Mwandishi Wetu - **MAGU**

Mgombea Urais wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli amesema kuwa mwaka 2015 wakati akiomba kura, alieleza nia ya kuleta mabadiliko ya kweli katika Wilaya ya Magu ambapo kwa kiwango kikubwa ametekeleza ahadi hizo.

Rais Magufuli amesema hayo aliposimama kuongea na wananchi wakati wa mkutano wake wa kuomba kura kwa wananchi wa Wilaya Magu, ambapo amesema jumla ya shilingi bilioni 5.5 zimetolewa kwa ajili ya kutoa elimu bure Wilayani Magu na ujenzi wa madarasa, maabara na maktaba umegharimu shilingi Bil.1.3.

"Tumefanya upanuzi wa hospitali ya Wilaya hapa Magu, tumejenga vituo vya afya viwili na ujenzi wa kingine kimoja unaendelea, tumekarabati zahanati 22 na kupeleka mashine ya X-Ray katika kituo cha afya Kisesa, miradi yote hii imegharimu shilingi bilioni.3.3," ameeleza Rais Dkt. Magufuli.

Akifafanua zaidi, Rais Magufuli amesema kuwa miradi mikubwa ya maji imetekelezwa kwa gharama ya shilingi bilioni 16 na mingine midogo midogo kwa shilingi bilioni 15.5. "Tumejenga barabara za lami za Wilaya hii kwa gharama ya shilingi bilioni 5.1 ikiwemo barabara ya Magu Mjini yenye urefu wa kilomita 5.7.

Aliongeza kuwa katika kipindi cha miaka mitano, Serikali ya Awamu ya Tano imefanikiwa kutoa mikopo isiyo na riba kutoka katika Halmashauri jumla ya shilingi milioni 377.8 ilitolewa kwa wanawake, vijana na walemavu.

Kwa upande wa ahadi zake kwa wananchi wa Wilaya ya Magu, Rais Magufuli amesema kuwa katika miaka mitano ijayo: "Tunaweza tukaamua kujenga bandari nyingine hapa Magu ili wananchi wa hapa waendeleo biashara zao, fedha zipo kwa sababu tuliwabana mafi-sadi," alisisitiza Rais Dkt. Magufuli.

Akizungumzia sekta ya viwanda, amesema kuwa wataendelea kufufua viwanda na kuendeleza vile vinavyotumia malighafi za ndani kama pamba ili tutengeneza nguo badala ya kupeleka nje marobota ya pamba. Kwa upande wa nishati katika Wilaya ya hiyo, Rais Magufuli amesema bado vijiji 38 tu ambavyo

bado havijafikishiwa umeme na kwamba endapo wananchi watamchagua katika Uchaguzi Mkuu vijiji vyote hivyo vitafikishiwa umeme.

Amewasisitiza wananchi kumchagua kuwa Rais kwa kipindi cha miaka mitano mingine kwani amejitoa kwa ajili ya kuwatumikia: "Kazi ya Urais ni kazi ya utumishi, madaraka haya akiyapata mtu asiyemtanguliza Mungu mbele atawapeleka wananchi pabaya. Nimekuwa Waziri kwa miaka 20, ninafahamu shida za watanzania", alisisitiza Dkt. Magufuli

Mgombea Urais wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli anaendelea na Kampeni zake katika mkoa wa Mwanza kwa kufanya mkutano mkubwa wa hadhara katika uwanja wa CCM Kirumba Septemba 7, 2020.





SIKUWAFUNGIA NDANI WAKATI WA COVID-19 ILI MSITSESEKE - MAGUFULI

Na Mwandishi Wetu - **MAGU**

Mgombea wa Urais kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama hicho, Rais Dkt. Pombe Magufuli amesema kuwa hakuweka 'Lockdown' wakati wa janga la Covid-19 kwa kuwa watazania wangeteseka na kuwa masikini.

Rais Magufuli amesema hayo leo Wilayani Magu aliposima kuongea na wananchi akiwa njiani kutoka Musoma kuelekea Mwanza ambapo kesho Septemba 7, 2020 atafanya mkutano mubwa wa

kampeni katika Uwanja wa CCM Kirumba.

Amesema kuwa wakati wa janga la ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya Corona, kulikuwa na masharti mengi kwa ajili ya kukabili ana na ugonjwa huo ikiwemo kuzuia watu kutoka nje ya nyumba zao (Lockdown), lakini yeye kama Kiongozi wa nchi alikataa masharti hayo kwa sababu watazania wangeteseka.

"Nilikataa masharti ya kufungia watu ndani kwa kuwa nilijua wananchi wangu mtapata tabu na wengi mngepoteza maisha kwa kuwa tunajua wenyewe maisha yetu yalivyo. Mwingine unataka ukatafute upate mlo wa siku wa familia halafu nikufungie, kwa kweli sikuwa tayari kuwadhuru wananchi wangu," anaeleza Rais Magufuli.

Mgombea huyo wa Urais kupitia CCM, aliwakumbusha maelfu ya wananchi hao, wakiwemo wazee, vijana na watoto namna baadhi ya wanasiasa walivyotumika kutaka kukwamisha bajeti ya maendeleo kwa kutoka Bungeni kwa madai ya kuwepo kwa Covid 19.

“Ndugu zangu, baadhi ya Wabunge wa upande ule mwingine, walitumika kama mawakala wa ‘wakubwa’, kutaka kukwamisha bajeti ya Serikali inayowaletea maendeleo na hata kutaka kuukwamisha uchaguzi huu mkuu.

Haya maendeleo mnayoyaona ni wabunge wa CCM waliosimama kidete na kuhakikisha vikao vya Bunge vinaendelea kama kawaida na kuhakikisha bajeti inapita kwenda kusaidia watanzania wote bila kuba-gua itikadi ya vyama vyao,” Rais Magufuli aliwaeleza wananchi hao.

Aidha, amewatahadharisha wananchi kuwa makini na wanasiasa

ambaoni ‘mawakala’ wa mabeberu ambao wanazunguka kuomba kura ili waweze kutumika vizuri na kutimiza matakwa ya wanaowatuma.

“Ndugu zangu uongozi haujaribiwi, msije mkafanya makosa ya siku moja yakaja kuwatesa kwa miaka mitano ijayo. Haya mnayoyaona sasa ni matokeo ya uamuzi wa busara mlioufanya siku moja miaka mitano iliyopita, kama mnavyoona mabadiliko katika sekta ya umeme, maji, afya, elimu na miundombinu ni uamuzi wenu wa oktoba 2015. Naomba mtuamini, tupeni ridhaa ya miaka mingine mitano mimi, Wabunge na Madiwani tuendeleo kuwatumikia kwa unyenyekevu. Nyie ndiyo waajiri wetu na ninawaahidi kuwa sitabweteka kwa kuwa najua bado kazi ipo kubwa ya kuleta maendeleo kwa watanzania wote,” aliongeza Dkt. Magufuli.

Pia Rais Magufuli amewasihi wananchi wa Wilaya ya Magu kutojisahau na kuridhika na amani iliyopo kwa kuwa CCM imeendelea kuienzi kwa kulinda ipasavyo.



SIRI YA AMANI TANZANIA NI UWEPO NA KUHESHIMIANA DINI MBALIMBALI NCHINI

Na Mwandishi Maalum - **ARUSHA**



Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa amesema siri ya Taifa la Tanzania kuen-delea kuwa na amani na kimbilio la watu wanaotoka katika nchi ambazo zimepoteza amani ni kwa sababu ya uwepo wa dini, hivyo amewapongeza viongozi wa dini zote nchini kwa kuen-delea kuliombea Taifa.

Majaliwa amesema kuwa kuanzia Serikali ya Awamu ya Kwanza hadi Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais Dkt. John Pombe Magufuli inaamini kwamba dini ni mkombozi na msingi mkubwa wa amani, mshikamano na utulivu uliopo nchini.

Waziri Mkuu ameyasema hayo leo Jijini Arusha katika kongamano maalumu lililoandalia na kituo cha Radio Safina kwa ajili ya kuliombea Taifa na viongozi wake wakati wa kuelekea kwenye uchaguzi mkuu. Kongamano hilo limefan-yika katika uwanja wa Magereza Kosongo, Arusha.

“Serikali itaendelea kushirikiana na dini zote na Rais Dkt. Magufuli anaamini kwamba dini inamchango mkubwa katika kulifanya Taifa kuendelea kuwa ana amani. Nawashukuru viongozi wa dini nchini kwa kuliombea Taifa na kulifanya liepukane na vikwazo vingi ambavyo vingeleta athari.”

Waziri Mkuu amesema nchi iliokolewa kutoka katika majanga mbalimbali ukiwemo ugonjwa wa corona ambao bado umeendelea kuyasumbua mataifa makubwa yenye uwezo na nguvu duni kutokana na maombi yaliyofanywa na dini zote baada ya Rais Dkt. Magufuli kuwaomba Watanzania wafunge siku tatu kumuomba Mwenyezi Mungu aliepushe Taifa na ugonjwa huo.

Ametumia fursa hiyo kuwasihi viongozi wa dini na wananchi kwa ujumla waendeleo kushirikiana katika kuliombea Taifa na wamuombe Mwenyezi Mungu aiepushe Tanzania na majanga ili nchi iendeleo kuwa na amani.

Akizungumzia kuhusu uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, 2020, Waziri Mkuu amesema siku ikifika wajitokeze kwa wingi na wakachague viongozi bora watakaoweza kuwaletia maendeleo katika maeneo yao.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Arusha Iddi Kimanta amewahakikishia wananchi wa mkoa huo kwamba mkoa upo salama na kwamba wajitokeze kwa wiki kushiriki katika kampeni na wasikubali kutishwa na mtu yeyote.

Mkuu huyo wa mkoa aliongeza kwa kuwasihi wananchi wa Arusha kamwe wasikubali kudanganywa na watu wasioutakia mema mkoa wao na Taifa kwa ujumla. "Tunzeni kadi zenu za kupigia kuwa ili wakati utakapofika muweze kuchagua viongozi bora."

Awali, Mama Hellen Lema ambaye ni Mkurugenzi wa Radio Safina iliyoandaa kongamano hilo amesema licha ya kuliombea Taifa na viongozi wake pia, kongamano hilo lililotanguliwa na maombi yaliyofanyika kwa siku 21 linalenga kuvunja madhabahu yaliyokuwa yanawakandamiza watu kwa muda mrefu.



MWANZA WAMKARIBISHA MAGUFULI KWA KISHINDO

Na Mwandishi Wetu - **MWANZA**



Unaweza kusema Mwanza wameamua kwenda na Dkt. John Pombe Magufuli, baada ya maelfu ya wananchi wa mkoa huo kukusanyika barabarani kila sehemu kwa ajili ya kumlaki Mgombea Urais wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Dkt. John Pombe Magufuli ambaye alikuwa akitokea mkoa wa Mara kwenda Mwanza.

Wananchi hao ambaop walijipanga katika maeneo mbalimbali ikiwemo Wilaya ya Magu, Igoma, Kisesa, Buzuruga, Nyamagana na Ilemela ambapo

Rais Magufuli alisimama maeneo yote hayo kuongea na wananchi waliokuwa wamejawa shauku ya kumuona Rais Magufuli.

Katika mikutano hiyo kuongea na wananchi waliokuwa wakimsubiri, Rais Magufuli anawaahidi wananchi kuwa wakimchagua tena ataipaisha Tanzania kutoka uchumi wa sasa wa kati kwenda uchumi wa juu zaidi kama ambavyo amefanikiwa kuifikisha Tanzania katika uchumi wa kati katika kipindi cha miaka mitano tu.

“Nawaomba Watanzania wote wa vyama vyote na hata wasio na vyama wanichague ili tuendeleze kazi hii tuliyoianza,” Rais Magufuli anawasihi wananchi wamchague ili afanye mabadiliko makubwa kwa Tanzania.

Aidha, amewaomba wananchi kuwachagua Wabunge na Madiwani wa CCM ili wakamsaidie katika kuendeleza kwa kasi harakati alizoanzisha za kuwaletea wananchi maendeleo katika sekta zote ikiwemo kiuchumi, afya, miundombinu, maji, elimu na uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Kwa mwitikio wa wananchi katika

maeneo yote aliyosimama baada ya wananchi kufunga barabara, ni dhahiri kuwa mgombea huyu sasa ameshapitishwa kwa kishindo na wakazi wa mkoa wa Mwanza.

Kesho Septemba 7, 2020 Rais Magufuli anatafanya Mkutano mkubwa katika uwanja wa CCM Kirumba ambapo mkutano huo utachagizwa na wasanii maarufu nchini kama Diamond Platnumz, Zuchu, Baraka The Prince, Chege, Mrisho Mpoto, Banana Zoro, Sholo Mamba, Lina Sanga, Kala Jere-maya na Young D, huku wakiongozwa na DJ anayekuja kwa kasi, DJ Sweet Lady kutoka Peramiho DJs.





KALI ZA MAGUFULI MKOANI MARA SEPTEMBER 5, 2020

- 1.** TULIPOKUJA KUOMBA KURA MWAKA 2015 TULIELEZA NIA YETU YA KULETA MABADILIKO YA KWELI KATIKA NCHI YETU, NIA YETU YA KUENDELEA KUFANYA MABADILIKO MAKUBWA KATIKA SEKTA MBALIMBALI BADO TUNAYO, TUPENI TENA MIAKA MINGINE MITANO TUKAENDELEE KUTEKELEZA.
- 2.** TUMETOA JUMLA YA SHILINGI BILIONI 6.8 KUGHARIMIA ELIMU BURE, AFYA TUMETOA BILIONI 3.3, MIRADI YA MAJI TUMETOA BILIONI 31.5, TU-MEJENGA BARABARA ZA LAMI ZA WILAYA YA MAGU KWA GHARAMA YA SHILINGI BILIONI 5.1, VIJIZI 38 TU NDIYO HAVIJAFIKISHIWA UMEME, TUMETOA JUMLA YA SHILINGI MILIONI 377.8 KWA AJILI YA MIKOPO ISIYO NA RIBA KWA WANAWAKE, VIJANA NA WALEMAVU.
- 3.** TUTAENDELEA KUFUFUA VIWANDA, TUNATAKA TUWE NA VIWANDA VYA KUTENGENEZA BIDHAA ZINAZOTOKANA NA MALIGHAFI ZA NDANI IKIWE-MO PAMBA ILI TUZALISHE NGUO BADALA YA KUPELEKA MAROBOTA YA PAMBA NJE YA NCHI.
- 4.** TANZANIA ILIKUA IKIHESABIKA NI NCHI MASKINI YA KUTUPA, LAKINI NDANI YA MIAKA MITANO TUPO KATIKA UCHUMI WA KATI, TUCHAGUENI TENA TUKAFANYE MAAJABU.
- 5.** KAZI YA URAIS NI KAZI YA UTUMISHI, MADARAKA HAYA AKIYAPATA MTU ASIYEMTANGULIZA MUNGU MBELE ATAWAPELEKA WANANCHI PABAYA. NIMEKUWA WAZIRI KWA MIAKA 20, NINAFHAMU SHIDA ZA WATANZANIA.



MAJALIWA: TUMEANDAA MAZINGIRA YA KUKUZA UCHUMI

Na Mwandishi Wetu - **MOSHI, KILIMANJARO**

Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa na Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa amesema Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais Dkt. John Pombe Magufuli imeandaa mazingira mazuri ya kuwawezesha Watanzania kujikwamua kiuchumi wakiwemo wafanyabiashara wadogo.

Mhe. Majaliwa amesema hayo leo alipohutubia mkutano wa kampeni uliofanyika katika Kata ya Kirima Juu Wilayani Moshi Mkoa wa Kilimanjaro wakati akimuomba kura Rais Dkt. John Pombe Magufuli na mgombea Ubunge wa Jimbo la Moshi Vijijini, Profesa Patrick Ndakidemi na wagombea Udiwani.

“Nimekuja hapa kuwaomba sana kura yenu ya ndio kwa Rais Dkt. Magufuli kwani mkiwa sehemu ya watanzania mnafahamu kazi kubwa ya kupeleka maendeleo aliyofanya nchi nzima bila ya ubaguzi wa aina yoyote, tuhakikishe tunampigia kura nyingi ili akaendeleze kazi aliyoitia,” ameeleza Majaliwa.

Akizungumzia kuhusu miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na Serikali katika HalPia, Mhe. Majaliwa amesema Serikali ya CCM imejenga miradi mingi ya kimkakati ikiwemo ya afya, maji, elimu, umeme, barabara, viwanja vya ndege kwa ajili ya kuboresha maendeleo ya Watanzaniaya. Serikali imetengeneza fursa katika maeneo mbalimbali zilizowezesha wananchi kujikwamua kiuchumi.

mashauri ya Wilaya ya Moshi, Waziri Mkuu amesema jumla ya shilingi bilioni 2.1 zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa Vituo cha Afya Uru Kyaseni, Uru Kusini na Okaoni pamoja na upanuzi na ukarabati wa zahanati za Kahe, Kilema, Kisao, Chemchemi, Mowo, Kitowo na Kituo cha Afya Shimbwe. Pia shilingi bilioni 12.2 zilitolewa kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi.

Kuhusu elimumsingi bila ada, Mhe. Majaliwa amesema Serikali imetoa shilingi bilioni 4.8 kwa ajili ya ukarabati, utawala, michezo, mitihani na posho kwa maafisa elimu kata na walimu wakuu katika shule za msingi 252 kwenye halmashauri ya wilaya ya Moshi.

“Serikali imetoa shilingi bilioni 10.2 kwa ajili ya fidia ya ada, chakula kwa shule za bweni na posho ya madaraka kwa Wakuu wa Shule katika shule za sekondari 59 kwenye halmashauri ya wilaya ya Moshi.”

Amesema shilingi bilioni 1.6 zimetumika kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa vyumba vya madarasa 18, matundu ya vyoo 109, bwalo moja, nyumba sita za walimu na jengo moja la utawala na ununuzi wa mashine ya kudurufu mitihani katika shule za msingi Maweni, Mahoma, Ngaroni na Saghana.

Pia, Waziri Mkuu amesema sh. bilioni 7.3 zimetumika kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa vyumba vya madarasa 26, matundu vyoo 45, maabara 14, mabweni sita na ujenzi wa nyumba za walimu katika shule za sekondari za Ashira, Umbwe, Sakayo Mosha na Muungano, Kisarika, Shimbwe na Kimochi.

Amesema Serikali imetoa shilingi bilioni 5.3 kwa ajili ya miradi mikubwa ya maji ya Lyamungo-Umbwe, Njiapanda, Tella Mande, Mamba-Mruma, Shimbi Mashariki, Leto na Ngareni. Pia imetoa shilingi bilioni 6.3 kwa ajili ya miradi mingine ya visima virefu ya Mweka, Mamba Kusini, Mang’ana, Kyaronga, Kiwaya na Rudugai, Kaloleni, Mkashilingi, Vyanzo vya Kipure, Nikodemo na Mrusungu.

Aidha Mheshimiwa Majaliwa alitumia jukwaa hilo kuvunja makundi ya wanachama wa CCM waliogombea nafasi ya ubunge na kuwaeleza wananchi kuwa Chama Cha Mapinduzi kina utaratibu wakati wa mchakato wa ndani, ambapo baada ya uteuzi wa chama wana-CCM wote huungana na kuwa kitu kimoja.

Jarida la Ni Magufuli Tena

2020 - 2025



Limeandaliwa na **TEAM MAGUFULI TENA**